

MKATABA WA UPANGAJI OFISI YA BIASHARA

MWENYENYUMBA: COSMOS CONSTRUCTIO LIMITED

MPANGAJI: MELAKA LOGISTICS LIMITED

~~h.~~

MKATABA WA UPANGAJI NYUMBA YA OFISI YA BIASHARA

Mkataba huu umetayarishwa leo tarehe09...../.....01...../2023

Mkataba wa upangaji umefanyika leo tarehe MKATABA HUU umefanyika leo tarehe09...../.....01...../2023 baina ya COSMOS CONSTRUCTION LIMITED S.L.P. 12288

Dar es salaam; (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "Mwenyenumba" kwa upande wa kwanza) na MELAKA LOGISTICS LIMITED ya S.L.P 12288, Dar es salaam; (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "Mpangaji" kwa upande wa pili);

Kwa kuwa Mwenyenumba anamiliki Nyumba na. 16 iliyopo ndani ya kiwanja na. 77, kitalu na. A, Barabara ya Siwa, eneo la Mikocheni Light Industrial, Kata ya Mikocheni, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam na ameamua kumpangisha Mpangaji kwa makubaliano kama yanavyoonekana hapo chini. Na kwa upande wa pili Mpangaji ameiona sehemu husika na ameridhia kupanga kwa madhumuni ya kufanya Ofisi ya biashara.

MTABA HUU UNASHUHUDIA MAKUBALIANO YAFUATAYO

1. Muda wa pango ni mwaka mmoja (miezi 12) tu kuanzia tarehe / / 2023 mpakaMwezi.....2024.
2. Kodi ya mwezi ni sh Shilingi Laki Moja tu (100,000/=Tsh) na Mpangaji tayari amelipa jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni Moja na Laki Mbili tu (1,200,000/=) kama kodi kwa muda wa mwaka mmoja wakati wa kusaini mkataba huu na Mwenyenumba anakiri kupokea kiasi hicho cha fedha.
3. Kwamba Mpangaji atazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za upangaji.
4. Mpangaji atatumia eneo husika kwa shughuli za kufanya Ofisi ya biashara tu. Pia Mpangaji anatakiwa kuhakikisha ulinzi na usalama wa mali zake katika kipindi chote cha mkataba.
5. Mpangaji hatakiwi kufanya matengenezo yoyote bila kibali cha Mwenyenumba, Mpangaji atafanya ukarabati mdogo wakati ukarabati mkubwa utafanywa na Mwenyenumba.
6. Mpangaji atatakiwa kulipa kodi ya pango kwa wakati muafaka.



7. Malipo ya umeme na maji ni juu ya Mpangaji.
8. Mpangaji atatakiwa kuhakikisha nyumba na mazingira yake yanakuwa safi, muda wote na atawajibika kuchangia ada ya usafi wa mazingira ya pamoja atakayokubaliana na Mwenyenyumba katika kipindi chote cha mkataba huu.
9. Mpangaji hataruhusiwa kupangisha mtu mwingine ofisi hiyo bila ridhaa ya Mwenyenyumba.
10. Notisi ya mwezi mmoja kwa kusudio la kuvunja mkataba, inaweza kutolewa na upande wowote wa mkataba huu.
11. Mpangaji atatakiwa kutoa notisi ya mwezi mmoja kabla ya Mkataba huu kwisha endapo atakua na nia ya kuendelea na mkataba kwa mwaka mwingine kwa masharti yatakayokubalika kwa wakati huo.
12. Endapo Mwenyenyumba hatakuwa na nia ya kumpangisha tena Mpangaji atawajibika kutoa notisi ya siku 30 kwa Mpangaji ya kuhama kwenye ofisi.
13. Mkataba huu utaongoza na Sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

1. MWENYE NYUMBA amekubaliana na MPANGAJI kama ifuatavyo:

- a) Mwenyenyumba atalipa kodi zote za serikali, kama kodi ya ardhi na majengo, na atawajibika na uharibifu wowote utakaosababishwa na majanga ya asili, na wakati huo kodi itakua imesitishwa hadi matengenezo yatakapokua yamekamilika.
- b) Mpangaji ambaye amelipa kodi na anatekeleza masharti yaliyoainishwa katika mkataba huu, ataitumia Ofisi bila bugudha na usumbufu wowote kutoka kwa Mwenyenyumba au mtu mwingine yoyote au mtu ambaye ameidhinishwa na Mwenyenyumba.

KWA KUSHUHUDIA MKATABA HUU pande zote mbili zimeweka sahihi katika tarehe na siku kama inavyoonekana hapa chini:-


UMETIWA SAHIHI na KUTOLEWA Dar es Salaam na
 SIMON MOGAMEMOREKA kwaniaba ya
 COSMOS CONSTRUCTION LTD ambaye namfahamu/
 ametambulishwa kwangu na LILIAN MUMUNYI
 ambaye namfahamu leo hii tarehe 09
 mwezi 01 mwaka, 2023

MWENYE NYUMBA



MBELE YANGU:

JINA: KELVIN NGELEJA
SAHIHI: [Signature]
CHEO: WAKILI
ANUANI: 34694



UMETTWA SAHIHI na KUTOLEWA Dar es Salaam na AHIMED MOHAMED BAGHOZAH kwaniaba ya MELAKA LOGISTICS LIMITED ambaye namfahamu/ametambulishwa

LILIAN M. MANGAZA
..... namfahamu leo hii tarehe 09 Mwezi 01.....2023

MPANGAJI

[Signature]

MBELE YANGU:

JINA: KELVIN NGELEJA
SAHIHI: [Signature]
CHEO: WAKILI
ANUANI: 34694

